TANGAZO LA SERIKALI Na. 84 la tarehe 17/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA MKATA YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kupanga Eneo La Mkata ya Mwaka 2023.

Kutangaza Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya Jumla na ya Kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo: -

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NP90 yenye majira - nukta 408635MS, 9351289KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa mto Mligazi hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NP31 yenye majira - nukta 425570MS, 9342537KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 2.8 katika uelekeo wa 223° 46' 58'' hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VTB292 yenye majira - nukta 427657MS, 9344805KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa umbali wa kilomita 8.8 katika uelekeo wa 287° 32' 18'' hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VTB117 yenye majira - nukta 436284MS, 9342073KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 1.3 katika uelekeo wa 193° 27' 30'' hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VTB 455 yenye majira - nukta 433653MS, 9347816KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 5 katika uelekeo wa 325° 16' 06'' hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VTB 296 yenye majira - nukta 433609MS, 9347899KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 8.11 katika uelekeo wa 19° 25' 22'' hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VTB 125 yenye majira - nukta 436360MS, 9355701KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini- Magharibi kwa kufuata uelekeo wa mto Mkula hadi unapokutana na mto Kwale; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki kwa kufuata uelekeo wa mto Kwale hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NP1 yenye majira - nukta 423649MS, 9364312KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 3.7 katika uelekeo wa 151° 17' 54'' hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira - nukta 421847MS, 9367636KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 4.8 katika uelekeo wa 203° 28' 55'' hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira – nukta 414820MS, 9363172KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 6.92 katika uelekeo wa 31° 45' 09'' hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VTB102 yenye majira – nukta 416088MS, 9357151KZ; hadi ulipoanzia".

Dodoma
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*